Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.31 - 2023

wizara_elimuTanzania  wizara_elimuTz  www.facebook/moestvt.com  www.wyestu.blogspot.com  www.moe.go.tz  ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

# Sasa Rasmi




# Wadau waahidi kuchangia elimu kwa zaidi ya Sh. bilioni 465






## - KAZI IENDELEE -

www.moe.go.tz




**BODI YA UHARIRI**

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
*Kamishna wa Elimu*

Atupele Mwambene
*Mkurugenzi wa Sera na Mipango*

Sylvia Lupembe
*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

Nelly Mtema
*Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN*

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja
Veronica Chitunda

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Nafasi ya wadau kuchangia kwenye Elimu

Nchi yoyote ili iweze kuendelea inashirikisha wadau katika masuala ya maendeleo, na nchi nyingi zilizoendelea ni zile zilizoshirikisha wadau katika mambo yake ikiwemo elimu hivyo uchangiaji wa masuala ya maendeleo duniani kote ni jambo lenye tija.

Vivyo hivyo Tanzania imekuwa ikishirikisha wadau katika kuchangia elimu na ndio maana Agosti 31, 2023 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliandaa hafla ya kutambua mchango wa wadau kwenye sekta ya elimu, kupitia mikoa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo chini ya Taasisi ya Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE).

Utambuzi huo unaonesha dhahiri kwamba Serikali inatambua mchango mkubwa wanaoutoa wadau na ina dhamira ya dhati ya kuendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha elimu ya mtoto wa kitanzania inakuwa bora.

Utayari wa Serikali unaonekana wazi pale inapoweka mazingira mazuri ya kila mdau wa elimu kuweza kuchangia kwenye elimu. Hii imeonekana pia kupitia Mfuko wa Elimu chini ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ambapo wachangiaji wamekuwa wakitambuliwa na kupewa hati maalum kutokana na mchango wao kwenye elimu. Hii ndio chachu kubwa kwa wadau kuendelea kuchangia.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda, Katibu Mkuu Prof. Carolyne Nombo kwa nyakati tofauti katika hotuba zao wamekuwa wakizungumzia juhudi za Serikali katika kuboresha elimu na kutambua kila wakati mchango wadau katika kufikia azma ya kutoa elimu bora

"Hakuna namna ya kukwepa kuwekeza kwenye elimu na kuwekeza kwenye elimu ni kuwekeza kwa vizazi na vizazi kwa hiyo Rais wetu alivyoongeza fedha kwenye elimu hakuangalia hakuangalia uchanguzi ujao anaangalia kizazi kijacho," Prof. Adolf Mkenda

"Tunawashukuru wadau kwa namna mavyowekeza kwenye elimu, niwaombe katika kutekeleza majukumu yenu muyafikie maeneo ambayo yamefikiwa kwa ucache au hajafikiwa kabisa badala ya kupeleka eneo moja mahitaji yanayofanana isipokuwa yanatekelezwa na wadau wawili tofauti," Prof. Carolyne Nombo

Cha kukumbukwa ni kwamba nchi yetu itajengwa na sisi watanzania na vivyo hivyo elimu yetu itaimarishwa na kuwa bora sisi wenyewe.

Heko kwa Wizara ya Elimu kwa kuendelea kutambua wadau wanaoendelea kuchangia katika ngazi mbalimbali za elimu.



Uwezeshaji Elimu >




# Wadau waahidi kuchangia elimu kwa zaidi ya Sh. bilioni 465

Tanzania kwa awamu mbili tofauti imenufaika na Mfuko wa kusaidia maendeleo ya elimu duniani kuanzia mwaka 2014 hadi sasa kwa kiasi cha sh bilioni 518.8 ambazo zimeelekezwa kwenye miradi ya elimu ya msingi.

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne ambae pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi iliyo chini ya Taasisi ya Ushirikiano wa elimu Duniani (GPE) Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amesema hayo kwenye Hafla ya Kutambua Mchango wa Wadau wa Sekta ya Elimu mkoani Dar es Salaam.

Dkt. Kikwete amesema awamu ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2014 hadi 2018 na ya pili ni mwaka 2019 hadi 2023. Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na fedha hizo katika awamu ya pili kuwa ni ujenzi wa madarasa ya shule za msingi 2,980, ujenzi wa matundu ya vyoo 7,673, nyumba za walimu 64, shule mpya 18 na mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalum 15.

Mengine ni ujenzi wa madarasa ya mfano ya elimu ya awali 300, ukarabati wa shule zenye vitengo vya elimu elimu maalum 13 na ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa kwa vituo vya walimu 252.

"Uboreshaji wa miundombinu hii umewezesha serikali kuimarisha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji shuleni kuendana na ongezeko la idadi ya wanafunzi," amesema Mhe. Kikwete

Alisema ufadhili wa GPE pia umewezesha upatikanaji wa jumla ya nakala za vitabu 36, 118,566 zilizochangia kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi mbalimbali za elimu ya msingi kwa kuimarisha ujifunzaji na upatikanaji wa maarifa.

Vilevile ufadhili huo umesaidia kuimarisha mfumo wa kutathimini ubora wa shule kwa ngazi ya awali na msingi pamoja na kusaidia utekelezaji wa mpango wa mafunzo endelevu kwa walimu kazini ambao umekuwa ni nyenzo muhimu katika kuimarisha utendaji wa kuboresha matokeo ya ujifunzaji kwa wanafunzi nchini.

Akizungumzia ahadi ziliotolewa na Wakuu wa Mikoa Mhe. Kikwete ametoa rai kwao kuhakikisha wanakamilisha ahadi hizo za zaidi ya Sh Bilioni 465 ili zisaidie nchi kupata fedha za ruzuku kiasi cha Dola milioni 50.

Kwa upande wake Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kutambua mchango wa wadau kwenye Sekta ya elimu ni kuendelea kuhimiza Sekta binafsi na wadau kushirikiana na Serikali ili kufanikisha utoaji wa elimu nchini pamoja na mageuzi ya elimu.

Amesema kuwekeza kwenye elimu ni nyenzo muhimu ya kusaidia nchi kwenda mbele na kwamba tofauti ya maendeleo ya nchi duniani haitokani kuwa na mafuta, madini na rasilimali za asili bali inatokana zaidi na watu wake kuelimika na kuweza katika kutumia sayansi, teknolojia

"Hakuna namna ya kukwepa kuwekeza kwenye elimu na kuwekeza kwenye elimu ni kuwekeza kwa vizazi na vizazi, kwa hiyo Rais wetu alivyoongeza fedha kwenye elimu haangalii uchaguzi ujao anaangalia kizazi kijacho,"amesema Prof. Mkenda.

Nae Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amewashukuru wadau wa elimu ambao kwa uzalendo wao wamechangia kwa dhati jitihada za Serikali kwa kuongeza bajeti ya Sekta ya elimu.

Prof. Nombo amesema mchango wa wadau hao umelenga kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu na kwamba hii inaashiria umoja na ushirikiano wa dhati uliopo katika kuboresha Sekta ya elimu

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila amemshukuru Rais Samia kwa namna anavyoboresha elimu katika mkoa huo na kwamba mpaka sasa mkoa huo unatekeleza miradi ya elimu yenye thamani ya Sh bilioni 85.

Elimu ni Maisha >

# 'Ukimnyima mtoto elimu unamnyima maisha'



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema elimu ndio mtaji na kwamba itabadilisha taifa liweze kusonga mbele.

Waziri Mkenda amesema hayo Mkoani Tanga alipokuwa akizindua Kampeni ya Niache Nisome Pangani Inanitegemea iliyobuniwa na Mkuu wa Wilaya ya Pangani Mhe. Zainabu Abdallah.

Amesema nchi inahitaji wataalam wazuri katika fani mbalimbali akitolea mfano madaktari, walimu na wahandisi ili iweze kusonga mbele hivyo ni vizuri kuwaacha watoto wasome ili waweze kutimiza ndoto zao.

"Elimu ni ufunguo wa maisha ukimnyima mtoto elimu unamnyima maisha, mafanikio ya watu waliosoma ni chachu katika kuleta mabadiliko," amesema Prof. Mkenda

Akizungumzia kampeni ya Niache Nisome Pangani Inanitegemea inayofanyika katika Halmashauri ya Pangani Mkoani Tanga Waziri Mkenda amempongeza Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe. Zainabu Abdallah pamoja na Mbunge wa Jimbo hilo Jumaa Aweso na kusema kuwa kuna la kujifunza kutoka katika halmashauri hiyo ili kuleta mageuzi ya elimu na amehimiza watu kujifunza kwenye mambo mazuri kama hayo.

Kufuatia ombi la Mhe. Aweso kuhusu VETA ya wilaya hiyo kuanza kutoa mafunzo Prof. Mkenda amemuahidi kuhakikisha VETA zote za Wilaya za Mkoa wa Tanga zinaanza kutoa mafunzo mwezi Septemba 2023.

Pia amesema kuwa kwa maelekezo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuweka Kampasi za Vyuo Vikuu katika mikoa 14 ambayo haina Vyuo hivyo, Tanga inakwenda kupata Kampasi ya Chuo Kikuu Mzumbe.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo Mhe. Husna Sekiboko amemuomba Waziri Mkenda kuupa Mkoa wa Tanga kipaumbele kwa fursa za elimu hasa wilaya ya Pangani kwa kuwa ni moja ya wilaya ambayo wanafunzi wanatembea umbali mrefu kufuata shule.

"Mhe. Waziri wanafunzi wanatembea umbali mrefu kuifuata shule katika wilaya hii, niliamua kutoa fedha zangu kuwaweka hostel kutokana na changamoto hiyo ili kuwaepusha na vishawishi njiani naomba fursa yoyote ikitokea ilete Pangani,"amesema Mhe. Sekiboko

Naye Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Jumaa Aweso amemshukuru Waziri Mkenda kwa kuwajengea VETA ya wilaya na kumuomba amfikishie salamu hizo kwa Mhe. Rais huku akimuomba kuifanya shule ya Funguni iliyopo wilayani humo kuwa na kidato cha tano na sita.

Naye Mkuu wa Wilaya hiyo Zainabu Abdallah amesema katika Halmashauri hiyo wameamua kuifanya elimu kipaumbele kutokana na wilaya hiyo kuwa nyuma kielimu na kwamba kupitia Kampeni waliyoianzisha ya Niache Nisome Pangani Inanitegemea halmashauri hiyo itakuwa na mageuzi makubwa kwenye elimu.

Kufanikisha mageuzi ya elimu >



# Ushiriki wa wadau katika kufanikisha mageuzi ya elimu ni muhimu - Nombo



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema Sekta ya Elimu ipo kwenye mageuzi makubwa ya elimu na hivyo kuhitaji wadau wengi kushirikiana na Serikali katika kufanikisha mageuzi hayo.

Prof. Nombo amesema hayo jijini Dodoma alipokutana na wawakilishi kutoka Benki ya Stanbic waliofika ofisi kwake kwa lengo la kutambulisha programu na bidhaa za benki zinazochangia maendeleo ya Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kuona namna ya kushirikiana katika utekelezaji wenye tija.

Amesema mwelekeo wa nchi kwa sasa ni kutoa elimu ujuzi ili kuzalisha nguvu kazi itayoweza kujiajiari na kuchangia katika maendeleo ya nchi.

" Nimefurahi sana kuwa tunazungumza lugha moja na wadau , jana tulikuwa na Benki moja ya hapa nchini na imesema inatoa mafunzo kwa vijana 5000 inatia moyo maana huu ndio mwelekeo wa nchi, sasa kupitia programu yenu ya uwekezaji kijamii (CSI) mnaweza kuona tutashirikiana vipi katika eneo hili na lile la kukuza ubunifu. Nashauri pia mkutane na OR-TAMISEMI ambao ni wamiliki na waendeshaji wa shule," amesema Prof. Nombo.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Prof. James Mdoe amewaomba kuangalia maeneo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa lengo la kuwaendeleza wabunifu wazawa lakini pia kusaidia wanafunzi wa vyuo vya kati na vyuo vikuu kupata elimu ya fedha.

Akizungumza katika kikao hicho Meneja Mawasiliano wa Benki ya Stanbic Doreen Diminic amesema lengo la kuwa na kikao na Wizara ni kuona maeneo ya kipaumbele ambayo Benki inaweza kushirikiana na Wizara pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha elimu ya mtoto wa kitanzania inakuwa bora.

Amesema tangu benki hiyo kuanza mwaka 1995 imekuwa pamoja na kufanya shughuli za kibiashara lakini kurejesha kwenye jamii kile wanachozalisha ikiwemo kununua madawati na kujenga miundombinu ya shule lakini pia kwa sasa benki imekuja na program ya National School Championship kwa ajili ya kutoa elimu ya ujasiriamali na fedha kwa wanafunzi.

"Mahali pote tulipo tunafocus kwenye elimu ndio kipaumbele cha Benki na ndio maana leo tumefika hapa Wizarani kuona namna tunavyoweza kushirikana, tunashukuru tumepata mwelekeo sahihi wa maeneo ya kuchangia," amesema Doreen.

## Kiswahili chashika kazi ng'ambo >

# Kiswahili kuanza kufundishwa Brazili

Lugha ya Kiswahili ikiwa ni moja ya lugha zinazotambuliwa kimataifa na kupewa siku ya kuadhimishwa, Nchi mbalimbali zimeanza kufundisha lugha hiyo na nyingine kujipanga kuanza kuifundisha ikiwemo nchi ya Brazil.

Hayo yamebainishwa jijini Dodoma wakati Balozi wa Tanzania nchini Brazil Mhe. Prof. Balozi Adelardus Kilangi alipokutana na kuzungumza na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda kuhusu utekelezaji wa azma hiyo nchini humo.

Akizungumza katika kikao hicho Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Vyuo Vikuu vina nafasi ya kutoa wataalamu wanaoweza kwenda kufundisha huku wakijiendeleza kimasomo.

Baadhi ya Vyuo vilivyopendekezwa kuingia kwenye mpango wa mwanzo wa kufundisha lugha ya Kiswahili nchini huko kwa utaratibu wa makubaliano kati ya Vyuo vya Tanzania na Vyuo vya Brazil ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ( UDSM) Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo Kikuu kimoja cha Binafsi kitakachopendekezwa.

"Mhe Balozi tunaomba usaidie kupata udhamini wa masomo nchini humo watu wetu waje wasome mafunzo mbalimbali ikiwemo ukalimani na lugha, Sayansi, Teknolojia na uhandisi huku wakiendelea kufundisha lugha ya Kiswahili ", amesema Prof. Mkenda

Kwa upande wake Balozi wa Tanzania nchini Brazil Mhe. Balozi Prof. Adelardus Kilangi amesema amefika nchini na ujumbe wake akiwa na agenda mbalimbali ikiwemo kushirikiana na Wizara kuhakikisha lugha ya Kiswahili inafahamika nchini Brazil.

Amesema lugha ya Kiswahili inatambulika rasmi hivyo Balozi zetu zimepaswa kuikuza lugha hiyo akisema nchi nyingi zimeanza kufundisha.


Ametaja baadhi ya mipango waliyo nayo katika kuikuza lugha ya Kiswahili nchini humo kuwa ni kuhakikisha inafundishwa kwenye moja ya Chuo Kikuu kilichopo katika mji wa Brasilia nchini humo ambacho kinafundisha lugha za Afrika.

Aidha amesema wataanzisha darasa ubalozini ili kutoa fursa kwa watu wengi zaidi kuendelea kujifunza lugha hiyo pamoja na kuanzisha " _Tanzania House"_itakayotangaza na kunadi utamaduni na bidhaa za Tanzania ikiwemo Kiswahili.

"Tayari tumepata fedha za kuanzisha Tanzania House katika mji wa SaoPaulo, tunataka kuona vitu vinavyotangaza utamaduni wa mtanzania vikiwekwa pale na kuendelea kuikuza pia lugha ya nchi yetu,"amesema Balozi Kilangi



Ufadhili miradi ya utafiiti >




# Shilingi bilioni 1.29 kutumika kwenye miradi ya utafiti

Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imetoa Sh. bilioni 1.29 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi saba ya kitafiti kutoka katika taasisi mbalimbali hapa nchini.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo na utoaji ufadhili huo kwa watafiti wanufaika wa miradi hiyo Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema fedha hizo zinatokana na tengeo katika bajeti kuu ya serikali pamoja na michango ya washirika wa maendeleo hususan Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Utafiti la Canada (IDRC) na Shirika la Maendeleo la Taifa la Norway (NORAD).

Amesema Serikali imeendelea kuongeza rasilimali fedha, kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kuvutia wadau wengine ndani na nje ya nchi kuwekeza katika shughuli za utafiti na ubunifu nchini.

"Mazingira rafiki yamewezesha Serikali katika kipindi cha miaka mitano (2019-2022), kugharamia jumla ya miradi 49 ya utafiti, iliyojumuisha zaidi ya watafiti 235 kutoka Taasisi za Elimu ya Juu na zile za Utafiti na Maendeleo nchini," amesema Prof Nombo

Ameongeza kuwa Taasisi 11 za Elimu ya Juu na Utafiti zimewezeshwa kukarabati na kununua vifaa vya maabara za utafiti na miundombinu mingine. Katika kipindi husika, kiasi cha Shilingi Bilioni 9.04 kimetumika katika kutekeleza matokeo hayo.

Akizungumzia matokeo ya utafiti utakaofanyika kupitia ufadhili uliotolewa Prof. Nombo amesema inatarajiwa kuimarisha ufaulu katika somo la hisabati kwa shule za msingi na sekondari, na kuongeza matumizi ya teknolojia zinazoibukia hususan matumizi ya akili bandia katika kuchagiza maendeleo katika sekta za Kilimo na Uvuvi, Afya, Elimu, na Manunuzi serikalini.

"Nimefarijika kuona tafiti zimejikita katika maeneo muhimu ya jamii na yanashirikisha sekta husika, kipekee niwapongeze TAKUKURU ambao mmeshirikiana na vyuo kuingia katika ushindani na kushinda kupata ufadhili Hivyo nasisitiza watafiti kuhusisha wadau wa sekta husika na tafiti mnazofanya na kuzingatia vipaumbele vya tafiti kitaifa( National Reserch Agenda)", Amesema Nombo

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dkt. Amos Nungu amesema kupitia mashirikiano hayo yaliyopo, COSTECH imefanikiwa kuleta fedha za utafiti hapa nchini zenye thamani ya takribani TZS. 9 bilion kwa kipindi cha miaka minne. Fedha hizi zimepitia COSTECH kwenda kwa watafiti wetu, na zingine zimeenda moja kwa moja kwao.

Ametaja baadhi ya maeneo yaliyonufaika na fedha hizi ni kuwa ni Uanzishwaji wa Vigoda viwili vya utafiti katika chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela (NM-AIST) Arusha na Tathmini ya madhara ya COVID19 kupitia MUHAS na UDOM.

"Nitoe wito kwa taasisi za utafiti na vyuo vikuu kuleta Tungo zao (proposals) kwenye eneo la usalama wa chakula. Mwisho wa kuwasilisha ni tarehe 10.09.2023 na kiasi cha fedha za kitanzania shilingi milion 650 zitatumika kufadhili miradi ya utafiti itakayoshinda,"amesema Dkt. Nungu.

Mafunzo kwa walimu >

# Walimu wa masomo ya ufundi wapewa mafunzo

Walimu wanaofundisha masomo ya ufundi nchini wanapatiwa mafunzo ili kuwaongezea mbinu za kuweza kufundisha masomo hayo kwa umahiri.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo mkoani Morogoro Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe amesema Wizara ipo kwenye mageuzi makubwa ya elimu ili iweze kutoa ujuzi hivyo mafunzo hayo ni katika kuwajengea uwezo walimu wa kuenenda na mageuzi hayo ya elimu.

"Elimu ya ufundi lazima ikimbizane na kasi ya mabadiliko ya teknolojia hivyo walimu mnapaswa kuwa chachu kwa wanafunzi kuvutika na masomo hayo kupitia mbinu mnazotumia kufundishia, amesema Prof. Mdoe

Amewataka walimu hao kuhakikisha wanatumia mbinu watakazozipata kuleta mageuzi katika ufundishaji wa masomo hayo na kuwafanya wanafunzi wapende kusoma masomo ya ufundi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Mafunzo ya elimu ya ualimu Huruma Magheni amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo walimu wa ufundi kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika ufundishaji ikiwemo kutumia zana mpya kama vishikwambi na kompyuta ambavyo vilitolewa hivi karibuni kwa walimu nchini kote.

Wakizungumza Kwa nyakati tofauti Walimu wa masomo ya ufundi walioshiriki mafunzo hayo wameishukuru Wizara kwa kuandaa mafunzo hayo kwa kuwa yatawasaidia kuboresha ufundishaji na hatimaye kuzalisha vijana wenye ujuzi.

Mafunzo ya walimu wanaofundisha masomo ya ufundi yanatolewa na Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu (TESP) unaofadhiliwa na Serikali ya Canada.





Maelekezo Kuboresha Elimu >



# Wadhibiti ubora nyinyi ndio jicho la wizara - Dkt Rwezimula

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula amewataka Wadhibithi Ubora wa Shule Nyanda za Juu Kusini kujiandaa kikamilifu kwenda sambamba na matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika ofisi hiyo.

Dkt. Rwezimula ametoa rai hiyo Agosti 9, 2023 wakati akizungumza na Watumishi Ofisi ya Udhibiti Ubora Nyanda za Juu Kusini mkoani Iringa, ambapo amesema suala la TEHAMA haliepukiki kwao na hivyo inawapasa kujielimisha vya kutosha kwenda sambamba.

"Sasa hivi tunaanza kusajili Shule kwenye mtandao, nyie mtakuwa wa kwanza, kwa maana maombi yataletwa kwenu, vile viambatisho vyote vya kukagua mtafanya nyinyi. Tutaleta mafunzo juu ya matumizi ya huo mfumo wa kusajili shule kwa mtandao" alisema Dkt. Rwezimula.

Dkt. Rwezimula amewata Watumishi hao kutambua kuwa wana jukumu la kusimamia kikamilifu miradi mbalimbali kwani serikali inatoa fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya madarasa na maabara kwa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.

"Sehemu nyingine tumekuta fedha matumizi yake sivyo, ujenzi wa Maabara haufuati michoro, Wadhibiti Ubora lazima mjue hilo ili kuisaidia serikali" alisema Dkt. Rwezimula.

Awali katika taarifa yake Mdhibiti Mkuu Ubora wa Shule Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mary Songorwa amesema kwa mwaka 2022/23 wamefanikiwa kufanya tathimini kwa Shule za Msingi 652 sawa na asilimia 54, shule za Sekondari 56 sawa na asilimia 56 pamoja na Vyuo vya Ualimu Vinne sawa na asilimia 57.

Ameongeza kuwa zoezi hilo limekwenda sambamba na kutoa ushauri kwa Walimu, wazazi pamoja na wenye shule Juu ya namna bora ya kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia.

Maendeleo endelevu ya Elimu >

# Mkenda azindua mwongozo wa kitaifa wa elimu kwa maendeleo endelevu 2023/2030




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kukamilika kwa Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu kwa Maendeleo Endelevu 2023/2030, ni ishara tosha kwa dunia kuwa Tanzania imejikita katika kutengeneza mazingira ya elimu yatakayochangia kwa kiasi kikubwa katika Maendeleo Endelevu ya taifa.

Prof. Mkenda ametoa kauli hiyo Septemba, 22, 2023 jijini Arusha katika hafla ya utiaji saini Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu kwa Maendeleo Endelevu 2023/2030, ambapo amesema Tanzania imefanikiwa kufika hatua hiyo, kufuatia makubaliano ya Mawaziri wa Elimu katika Nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), katika kuidhinisha maandalizi ya Mwongozo wa namna ya kuwa na elimu inayondana na mahitaji ya Maendeleo Endelevu katika nyanja mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi.

"Tunafurahi kwamba hatimaye sisi tuna mwongozo, na inawezekana ndio nchi ya kwanza ya SADC kukamilisha kazi hii. Tunaishukuru sana UNESCO na UNICEF kwa kazi kubwa waliyoifanya, pamoja Wizara mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar zilizoshiriki katika maandalizi ya mwongozo huo" amesema Prof. Mkenda.

Aidha Prof. Mkenda ameeleza kuwa Mwongozo huu una akisi masuala yote yaliyopo kwenye rasimu ya Sera ya elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023, na kwamba elimu ambayo itakuwa inatolewa ya mafunzo ya Amali itawaandaa vijana kikamilifu katika maeneo mbalimbali ikiwemo kilimo.

"Ni ahadi kwa watoto wetu na vizazi vijavyo kwamba tumejitolea kuwapa elimu bora zaidi, ambayo inawapa maarifa na maadili yanayohitajika katika ulimwengu unaobadilika haraka huku tukikuza hisia ya uwajibikaji kwa mazingira na jamii". Alibainisha Prof. Mkenda

Akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Salum Abdallah, amesema mwongozo huo umekuja wakati muafaka, wakati Zanzibar ikiendelea kufanya maboresho ya Mitaala Elimu.

"kutoka kwenye Mitaala ya maarifa tunaingia kwenye Mitaala ya umahiri ambayo tunaamini kabisa itaweza kumjenga mwanafunzi kutumia maarifa wanayoyapata kwa ajili ya kutatua changamoto zao mbalimbali za kimazingira, kijamii pamoja na kuwapatia maendeleo ya kiuchumi" Alisema Abdallah.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) Michel Toto ameishukuru Serikali kuendeleza kushirikiana na UNESCO, huku akiwataka Wadau wa Maendeleo kuunga mkono juhudi hizo zinazolenga kutekeleza kwa pamoja mkakati huo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Tunaishukuru serikali ya Tanzania kupitia wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hapa Tanzania Bara na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, kwa nia yake ya dhati kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya mwongozo huu wa kimkakati. Mwongozo huu unaakisi matarajio yetu ya pamoja kwenye elimu ya baadaye katika taifa hili" alisema Toto.

Aidha Toto amelishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto na (UNICEF) kwa msaada wa Kifedha ambao umesaidia kuratibu maandalizi ya mwongozo huo katika ngazi mbalimbali.



# Uwekezaji zaidi vifaa VETA >



## Kamati ya Kudumu ya Bunge yashauri Serikali kuwekeza vifaa zaidi VETA Kagera

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu Utamaduni na Michezo imeiagiza serikali kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuhakikisha inawekeza vifaa muhimu vya kujifunzia katika chuo cha Veta Kagera ili kuunga mkono maono ya Rais Dkt. Samia Suluh Hassan.

Agizo hilo limetolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Husna Juma Sekiboko Mbunge wa Viti Maalum kutoka mkoa wa Tanga aliyeongoza kamati hiyo na kufika chuoni hapo ambapo wamekagua na kujionea hali halisi na namna wanafunzi wanavyojifunza.

Ametumia fursa hiyo kumpongeza na kumshukuru Dkt. Samia Suluh Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwekeza fedha nyingi kwenye ujenzi wa vyuo vya Veta nchini ili kuweza kuwasaidia watanzania walio wengi ambao walikuwa wakikosa fursa ya kupata hata elimu ya ujuzi.

Ameitaka wizara ya elimu kuyaishi maono hayo ya Mama Samia kwa kuacha kuwafundisha wanafunzi kwa Nadharia na badala yake waweke vifaa vya kujifunzia ili watoto wanapotoka kwenye vyuo hivyo wawe na uwezo wa kujiajiri na sio kutangatanga tena mitaani kutafuta ajira.

Wakizungumza kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati hiyo baadhi ya wabunge ambao ni Mwl. Aloyce Kamamba Mbunge wa Buyungu Kakonko ameipongeza serikali kwa uwekezaji mkubwa wa chuo kikubwa cha Veta Kagera na kusema kuwa kwenye vyuo vya Veta ndiko kunapatikana mafunzo yakumaliza changamoto kwa wananchi na kuongeza kuwa serikali iendelee kuwekeza vifaa pamoja na wahitimu kupewa fedha kama mtaji.

Kwa upande wake naibu waziri wa Elimu sayansi na teknolojia Mhe. Omary Kipanga na Mbunge wa Jimbo la Mafia amesema kuwa wizara imepokea maelekezo yote yaliyotolewa na kamati na kuahidi kuyafanyia kazi kwa haraka ili kutimiza malengo ya serikali.

Hata hivyo baadhi ya wananfunzi wanaosoma kwenye chuo hicho wameishukuru serikali kwa kujenga chuo hicho ambacho kimetoa fursa kwa vijana ambao walikuwa vijijini na sasa wanapata ujuzi huku wengine wakiomba serikali kutoa fursa ya vijana hao kupata mikopo ili kuweza kupunguza ukali wa maisha hasa wawapo chuoni.

Chuo cha Veta Kagera kilichojengwa kwa ufadhili wa serikali ya China kwa gharama ya shilingi bilioni 22 katika kata Nyakato Halmashauri ya wilaya Bukoba kina uwezo wa kuwahudumia wanafunzi zaidi ya 400 wa Bweni.



## NUKUU >

**"TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA"**

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engututo, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz